

Do Your Part with All Your Heart

By Elder Dieter F. Uchtdorf
Of the Quorum of the Twelve Apostles

Fanya Sehemu Yako kwa Moyo Wako Wote

Na Mzee Dieter F. Uchtdorf
Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

October 2025 general conference

Trust the Savior and engage, patiently and diligently, in doing your part with all your heart.

Last year during a trip to Europe, I visited my old place of employment, Lufthansa German Airlines at the Frankfurt Airport.

To train their pilots, they operate several sophisticated full-motion flight simulators that can re-create almost any normal and emergency flight condition. During my many years as an airline captain, I had to pass a check flight in the flight simulator every six months to keep my pilot license current. I remember well those intense moments of stress and anxiety but also the feeling of accomplishment after passing the test. I was young then and loved the challenge.

During my visit, one of the Lufthansa executives asked if I would like to give it a try again and fly the 747 simulator one more time.

Before I had time to fully process the question, I heard a voice—sounding astonishingly like my own—saying, “Yes, I would like that very much.”

As soon as I said the words, a tsunami of thoughts flooded my mind. It had been a long time since I flew a 747. Back then I was young and a confident captain. Now I had a reputation to live up to as a former chief pilot. Would I embarrass myself in front of these professionals?

But it was too late to back down, so I settled into the captain’s seat, placed my hands on the familiar and beloved controls, and felt, once again,

Mtumainie Mwokozi kujihusisha, kwa subira na bidii, katika kufanya sehemu yako kwa moyo wako wote.

Mwaka jana wakati wa safari huko ulaya nilitembelea sehemu yangu ya zamani ya ajira Lufthansa German Airlines huko Uwanja wa Ndege wa Frankfurt.

Ili kuwafunza marubani wake, waliendesha mafunzo ya kisasa ya kuigiza ya kuendesha ndege ambayo yanaweza kutengeneza karibia hali yoyote ya kawaida au ya dharura kwenye ndege. Wakati wa miaka yangu mingi kama rubani wa ndege, ilinibidi kufaulu mtihani wa urubani katika mashine ya kuigiza kuendesha ndege kila baada ya miezi sita ili leseni yangu ya urubani ibaki hai. Nakumbuka vyema nyakati hizo ngumu za shinikizo na hofu lakini pia hisia ya mafanikio baada ya kufaulu mtihani. Nilikuwa kijana kipindi hicho na niliipenda changamoto hiyo.

Wakati wa matembezi yangu, mmoja wa watendaji wa Lufthansa aliomba kama naweza kujaribu tena kuendesha ndege ya 747 kwenye mashine ya kuigiza.

Kabla ya kuchakata jambo hili kikamilifu, nilisikia sauti—ikinijia kwa kushangaza kama ya kwangu—ikisema, “Ndio, ningependa hilo sana.”

Mara tu niliposema maneno hayo, wingi wa mawazo ulifurika akili yangu. Ni kitambo sasa tangu niendeshe 747. Wakati ule nilikuwa kijana na rubani jasiri. Sasa nilikuwa heshima ya kutunza kama rubani mkuu aliyestaafu. Je, nitajiaibisha mwenyewe mbele ya wabobezi hawa?

Lakini tayari haikuwezekana kukataa, hivyo nilikaa kwenye kiti cha rubani, nikaweka mikono yangu kwenye gia ninazozifahamu na pendwa,

the exhilaration of flight as the big jet roared down the runway and took off into the wild blue yonder.

I'm happy to say that the flight was successful, the aircraft remained intact, and so did my self-image.

Even so, the experience was humbling for me. When I was in my prime, flying had become almost second nature. Now it took all my concentration to do the basic things.

Discipleship Takes Discipline

My experience in the flight simulator was an important reminder that getting good at anything—whether it be flying, rowing, sowing, or knowing—takes consistent self-discipline and practice.

You might spend years acquiring a skill or developing a talent. You might work so hard that it becomes second nature to you. But if you think that means you can stop practicing and studying, you'll gradually lose the knowledge and abilities you once acquired at great cost.

This applies to skills like learning a language, playing a musical instrument, and flying an airliner. It also applies to becoming a disciple of Christ.

Simply put, discipleship takes self-discipline.

It is not a casual endeavor, and it doesn't happen by accident.

Faith in Jesus Christ is a gift, but receiving it is a conscious choice that requires a commitment of all our "might, mind and strength." It is a practice of every day. Every hour. It takes constant learning and determined commitment. Our faith, which is our loyalty to the Savior, becomes stronger as it is tested against the opposition we face here in mortality. It endures because we keep nourishing it, we keep actively applying it, and we never give up.

On the other hand, if we fail to use faith and its convincing power by acting upon it, we become less sure of things we once held sacred—less confident of things we once knew were true.

Temptations that would never have enticed us begin to look less appalling and more appealing.

The fire of yesterday's testimony can warm us for only so long. It needs constant nourishment

na kuhisi, kwa mara nyingine, utamu wa urubani wakati ndege kubwa ya 747 ikikimbia kwenye njia na kupaa kwenye anga ya buluu na mbali.

Ni furaha kusema kwamba safari hii ilifanikiwa, ndege ilibaki salama, vivyo hivyo na taswira yangu.

Hata hivyo, uzoefu ulikuwa wa kunyenyekeza kwangu. Nilipokuwa kijana, kuendesha ndege ilikuwa kama jambo lililozoeleka. Sasa, inachukua jitihada zangu zote kufanya vitu vya msingi.

Uanafunzi Huhitaji Nidhamu

Uzoefu wangu kwenye mashine ya urubani ilikuwa ni ukumbusho muhimu kwamba kuwa bora kwenye chochote—iwe kupaisha ndege, kupiga kasia, kupanda au kujua—huhitaji nidhamu binafsi na mafunzo endelevu.

Unaweza kutumia miaka mingi ya kupata ujuzi au kukuza talanta. Unaweza kufanya kazi kwa bidii hadi izoeleke kwako. Lakini kama unafikiri hiyo inamaanisha uache kufanya mazoezi na kujifunza, taratibu unapoteza maarifa na uwezo ambao uliupata hapo awali kwa gharama kubwa.

Hii ni kwa ujuzi kama kujifunza lugha, kupiga kifaa cha muziki na kuendesha ndege. Pia inatumika katika kuwa mwanafunzi wa Kristo.

Kwa neno jepesi, uanafunzi huhitaji nidhamu.

Sio juhudi ya kawaida, na haitokei kwa ajali.

Imani katika Yesu Kristo ni zawadi, lakini kuipokea inahitaji uchaguzi wa dhahiri ambao unahitaji dhamira ya "uwezo, akili na nguvu" zetu zote. Ni tendo la kila siku. Kila saa. Inahitaji mafunzo ya mara kwa mara na dhamira madhubuti. Imani yetu, ambayo ni utiifu wetu kwa Mwokozi, huwa imara pale inapojaribiwa dhidi ya upinzani tunaokutana nao hapa duniani. Imani hustahimili kwa sababu tunaendelea kuilisha, kuendelea kuitumia na kutokata tamaa.

Kwa upande mwingine, ikiwa tunashindwa kutumia imani na na nguvu zake za kusadikisha, tunakuwa na uhakika dhaifu wa vitu tulivyoviona vitakatifu—ujasiri hafifu kwa vitu tulivyojua awali kuwa kweli.

Majaribu ambayo kamwe hayangeweza kutuvutia yanaanza kuonekana ya kuogofya tu kidogo na ya kuvutia zaidi.

Makali ya moto wa ushuhuda wa jana unatupatia joto kwa muda tu. Makali hayo yana-

to keep burning brightly.

In the New Testament, the Savior taught a parable about a master who gave each of his servants a sacred trust—a quantity of money called talents. The servants who diligently used their talents increased them. The servant who buried his talent eventually lost it.

The lesson? God gives us gifts—of knowledge, of ability, of opportunity—and He wants us to use and amplify them so they can bless us and bless His other children. That doesn't happen if we put those gifts high on a shelf like a trophy that we admire from time to time. Our gifts magnify and multiply only when we put them to use.

You Are Gifted

“But Elder Uchtdorf,” you might say, “I don't have any gifts or talents—at least, none that are that valuable.” Perhaps you look at others whose gifts are obvious and impressive and you feel pretty ordinary by comparison. You might suppose that in the premortal existence, on the day of the great gift and talent smorgasbord, your plate seemed woefully sparse—especially compared to the stacked and overflowing plates of others.

Oh, how I wish I could embrace you and help you understand this great truth: You are a blessed being of light, the spirit child of an infinite God! And you bear within you a potential beyond your own capacity to imagine.

As poets have noted, you come to earth “trailing clouds of glory”!

Your origin story is divine, and so is your destiny. You left heaven to come here, but heaven has never left you!

You are anything but ordinary.

You are gifted!

In the Doctrine and Covenants, God declared:

“There are many gifts, and to every [person] is given a gift by the Spirit of God.

“To some is given one, and to some is given another, [and] all may be profited thereby.”

Some of our gifts are listed in the scriptures. Many are not.

As the prophet Moroni said, “Deny not the gifts of God, for they are many; and they come from the same God.” They might manifest themselves in “different ways ... ; but it is the same

hitaji lishe endelevu ili kuendelea kuwa angavu.

Katika agano jipya, Mwokozi anafundisha mfano kuhusu bwana aliyempa kila mtumishi wake tumaini tukufu—kiasi cha pesa kiitwacho talanta. Watumishi waliotumia kwa bidii talanta zao walizikuza. Mtumishi ambaye alizika talanta yake hatimaye aliipoteza.

Somo la kujifunza? Bwana anatupatia vipawa—vya maarifa, vya uwezo, vya fursa—na anatatuka kuvitumia na kuvikuza ili vitubariki sisi na kuwabariki watoto Wake wengine. Hiyo haita-tokea kama tukiviweka juu ya kabati kama tuzo ya kutamania kila wakati. Vipawa vyetu hukua na kuongezeka pale tunapovitumia tu.

Wewe una Kipawa

“Lakini Mzee Uchtdorf,” unaweza kusema, “sina kipawa au talanta—angalau chenye thamani hiyo.” Labda unawaangalia wengine ambao vipawa vyao ni dhahiri na vinavutia na unahisi wewe ni wa kawaida tu. Unaweza kudhani kwamba katika maisha kabla ya hapa duniani, katika karamu ya siku ya vipaji vikuu na talanta, sahani yako ilionekana ina kidogo—hasa ukilinganisha na sahani za wengine zilizosheheni na kumwagika.

Ee, ni kiasi gani natamani ningekukumbatia na kukusaidia kuelewa ukweli huu mkuu: Wewe ni binadamu wa nuru uliyebarikiwa, mwana wa kiroho wa Mungu asiye na mwisho! Na unabeba ndani yako uwezekano zaidi ya uwezo wako wa kufikiria.

Kama washairi walivyosema, unakuja duni-ani kwa “utukufu binafsi wa uungu”!

Chanzo cha hadithi yako ni kitukufu, vivyo hivyo na mwisho wako. Uliondoka mbinguni kuja hapa, lakini mbingu kamwe hazijakuacha!

Wewe ni zaidi ya mtu wa kawaida.

Wewe una kipawa!

Katika Mafundisho na Maagano, Mungu anatangaza:

“Kwani kuna vipawa vingi, na kwa kila [mtu] kipawa kimetolewa na Roho wa Mungu.

“Kwa wengine wamepewa kimoja, na wengine wamepewa kingine, [na] wote waweze kufaidika.”

Baadhi ya vipawa vyetu vimeorodheshwa katika maandiko. Vingi havipo.

Kama nabii mkuu Moroni alivyosema, “Msikatae karama za Mungu, kwani ni nyingi; na zinatoka kwa yule yule Mungu.” Vinaweza kujidhihirisha katika “njia tofauti ... ; lakini ni yule

God who worketh all in all.”

It may be true that our spiritual gifts are not always flashy, but that does not mean they are less important. May I share with you some spiritual gifts that I have noticed in so many members across the world? Contemplate whether you have been blessed with one or more gifts like:

Showing compassion.
Noticing people who are overlooked.
Finding reasons to be joyful.
Being a peacemaker.
Noticing small miracles.
Giving sincere compliments.
Forgiving.
Repenting.
Enduring.
Explaining things simply.
Connecting with children.
Sustaining Church leaders.
Helping others know that they belong.

You might not see these gifts displayed at the ward talent show. But I hope you can see how precious they are to the Lord’s work and how you might have touched, blessed, or even saved one of God’s children by your gifts. Remember: “By small and simple things are great things brought to pass.”

So let us each do our little part.

Do Your Little Part

My beloved brothers and sisters, dear friends, I pray that the Spirit will help you recognize the gifts and talents God has given you. Then, let us, like the faithful servants in the Lord’s parable, increase and magnify them.

The day will come when we stand before our compassionate Father in Heaven to give an account of our stewardship. He will want to know what we did with the gifts He gave us—in particular, how we used them to bless His children. God knows who we truly are, who we are designed to become, and so His expectations for us are high.

But He doesn’t expect us to take some grand, heroic, or superhuman leap to get there. In the world He created, growth happens gradually and patiently—but also consistently and unrelentingly.

Remember, it is Jesus Christ who already did the superhuman part when He conquered death

yule Mungu azitendaye kazi zote katika wote.”

Inaweza kuwa kweli kwamba vipawa vyetu vya kiroho daima sio vya kuvutia, lakini hiyo haimaanishi si vya muhimu. Je, naweza kushiriki nanyi baadhi ya vipawa vya kiroho ambavyo nimeviona kwa waumini ulimwenguni kote? Tafakari kama umebarikiwa na moja au zaidi ya vipawa kama:

Kuonyesha huruma.
Kuwatambua watu ambao hawatambuliki.
Kutafuta sababu ya kuwa na shangwe.
Kuwa mpatanishi.
Kutambua miujiza midogo.
Kutoa maneno ya dhiti ya kusifu.
Kusamehe.
Kutubu.
Kuvumilia.
Kuelezea vitu kwa urahisi.
Kuunganika na watoto.
Kuwakubali viongozi wa Kanisa.
Kuwasaidia wengine kuwa sehemu ya kitu.

Unaweza usione vipawa hivi vikionyesha kwenye maonyesho ya vipaji ya kata. Lakini natumaini mnaweza kuona jinsi vilivyo vya thamani kwenye kazi ya Bwana na jinsi unavyoweza kumgusa, kumbariki au hata kumwokoia mmoja wa watoto wa Mungu kwa kipawa chako. Kumbuka: “Kupitia vitu vilivyo vidogo na rahisi vitu vikubwa hutendeka.”

Basi tufanye kila mmoja sehemu yetu ndogo.

Fanya Sehemu Yako Ndogo

Wapendwa kaka na dada zangu, marafiki wapendwa, naomba Roho atakusaidia kutambua vipawa na talanta ambazo Mungu amekujalia. Kisha, acha sisi, kama watumishi waaminifu kati ka mfano wa Bwana, tuviongeze na kuvikuza.

Siku itakuja tutakaposimama mbele ya Baba yetu wa Mbinguni mwenye huruma kutoa maelezo ya uwajibikaji wetu. Atahitaji kujua tulifanyia nini vipawa alivyotupatia—hasa, jinsi tulivyovitumia kubariki watoto Wake. Mungu anatumia sisi ni nani, tumesanifiwa kuwa nani na matarajio Yake kwetu yako juu.

Lakini Yeye hatarajii sisi kupiga hatua kubwa, ya kijasiri au ya kuzidi binadamu ili kufikia hapo. Katika ulimwengu alioumba, ukuaji hutokea taratibu na kwa uvumilivu—lakini pia ni endelevu na usiokoma.

Kumbuka, ni Yesu Kristo ambaye amekwishafanya sehemu ya kuzidi binadamu wakati

and sin.

Our part is to follow the Christ. It is our part to turn away from sin, turn toward the Savior, and walk in His way, one step at a time. As we do this, diligently and faithfully, we eventually cast off the shackles of imperfections and faults and slowly become refined, until that perfect day when we will be perfected in Christ.

The blessings are within reach. The promises are in place. The door is wide open. It is our choice to enter and begin.

The beginning may be small. But that is OK.

Where faith is weak, begin with a hope in Christ Jesus and in His power to cleanse and purify.

Our Father asks that we approach this challenge of faith and discipleship not as casual tourists but as wholehearted believers who leave behind and abandon Babylon and set their hearts, minds, and steps toward Zion.

We know that our efforts alone cannot make us celestial. But they can make us loyal and committed to Jesus the Christ, and He can make us celestial.

Because of our beloved Savior, there is no such thing as a no-win scenario. If we place our hope and faith in Him, our victory is assured. He promises us access to His strength, His power, His abundant grace. Step by step, little by little, we will grow ever closer to that great and perfect day when we will live with Him and our loved ones in eternal glory.

To get there, we must do our part today and every day. We are thankful for the steps we took yesterday, but we don't stop there. We know we still have a long way to go, but we don't let that discourage us.

That is the essence of who we are—as followers of Christ.

I urge and bless every member of the Church, and all who desire to be part of it, to trust the Savior and engage, patiently and diligently, in doing your part with all your heart—that your joy may be full and that, one day, you will receive all the Father has. Of this I bear witness in the name of Jesus Christ, amen.

aliposhinda kifo na dhambi.

Sehemu yetu ni kumfuata Kristo. Ni sehemu yetu kugeuka kutoka dhambini, kumgeukia Mwokozi na kutembea njia Yake, hatua moja kwa wakati. Tunapofanya hivi, kwa bidii na kwa uaminifu, hatimaye tunaondokana na pingu za kutokuwa wakamilifu na makosa na taratibu tunatakaswa, mpaka siku ile kamilifu tutakayokamilishwa ndani ya Kristo.

Baraka ziko ndani ya uwezo wetu. Ahadi zipo tayari. Mlango umefunguliwa. Ni chaguo letu kuingia na kuanza.

Mwanzo unaweza kuwa mdogo. Lakini hiyo ni SAWA.

Pale ambapo imani ni dhaifu, anza na tumaini katika Kristo Yesu na nguvu Yake ya kusafisha na kutakasa.

Baba yetu anatuomba tufanye changamoto hii ya imani na uanafunzi si tu kama watalii wa kawaida lakini kama waaminio wa dhati, ambao wanaiacha babilonia na kuweka mioyo yao, akili na hatua kuelekea Sayuni.

Tunajua kwamba jitihada zetu pekee haziwezi kutufikisha selestia. Lakini zinaweza kutufanya waaminifu na wenye kudhamiria kwa Yesu Kristo, na Yeye atufikisha selestia.

Kwa sababu ya Mwokozi wetu mpendwa, hakuna kitu kama tukio lisilo la mafanikio. Kama tukiweka tumaini na imani yetu Kwake, ushindi wetu ni wa uhakika. Ametuahidi kufikia nguvu Zake, uwezo Wake, neema Yake tele. Hatua kwa hatua, kidogo kidogo, tutasonga karibu zaidi na siku hiyo kuu na kamilifu tutakapoishi pamoja Naye na wapendwa wetu katika utukufu wa milele.

Ili kufika hapo, lazima tufanye sehemu yetu leo na kila siku. Tuna shukrani kwa hatua tulizopiga jana, lakini tusikwamie hapo. Tunajua bado tuna njia ndefu ya kusonga, lakini haturuhusu hilo litukatishe tamaa.

Hicho ndicho kiini cha sisi ni nani—kama wafuasi wa Kristo.

Ninawasihi na kumbariki kila muumini wa Kanisa, na wote wanaotamani kuwa sehemu yake, kumwamini mwokozi na kujihusisha, kwa uvumilivu na kwa bidii, katika kufanya sehemu yako kwa moyo wako wote—ili furaha yako iwe kamilifu na kwamba, siku moja, utapokea vyote alivyonavyo Baba. Juu ya hili ninashuhudia katika jina la Yesu Kristo, amina.